BARUA KWA DR. MUHAMMAD BIN HĀDĪ KUHUSU ONYO LAKE DHIDI YA SHEIKH SĀLIH AS-SINDĪ

SHEIKH SĀLIM AT-TWAWÎL (HAFIDHAHULLĀH)

Kila Sifa njema zinamstahiki Allâh, na twamuomba amfikilizie Swala na Salamu yule ambaye hakuna Mtume mwengine atakayekuja baada yake, Amma ba'd:

Zimenifikia mimi habari, kama zilivyowafikia wengine, yakwamba Sheikh, Dr Sālih bin 'Abdul'Azeez as-Sindī atafanya ziyara katika Mji wa Dubai na baadhi ya ndugu wamemualika ili atoe mafunzo hapo juu ya 'Aqîda katika miongoni mwa Nyumba za Allâh, Allâh amuafikie katika kheri na amja'aliye kufuzu kwenye yaliyo na kheri kwa waja na miji, na twamuomba Allâh atufaidishe kwa kupitia kwake kwa wanafunzi wa ki-ilimu na amfanye yeye kuwa ni mwenye kutuongoza. Mimi simjui Sheikh Sālih as-Sindī, katika maishani mwangu niliwahi kumuona mara moja tu kwenye karamu ya jioni tukiwa pamoja na Sheikh Falāh bin Ismā'îl Mandikār, Allâh Amuhifadhi. Tuliamkuana bila ya kuzungumza ya zaidi, lakini hatahivyo, yeye ni mtu maarufu mbele ya ma-'Ulamaa' kwani yeye ni profesa katika Chuo Kikuu Cha Ki-Islamu Cha Madinah katika idara ya 'Aqîdah. Ma-'Ulamaa' wengi wanamjua yeye na wamemsifu na kumtaja kwa kheri, ana vitabu vizuri na vyenye faida kubwa katika Aqîdah tena ni vitabu vilivyoenea sehemu nyingi na vilivyo mashuhuri. Anatembelea Nchi nyingi na ana mipangilio mizuri na shughuli nzuri za ki-Da'wah, Allâh Amuafikie kwenye kheri na Ambariki.

Nimewahi kuona, kama walivyo ona wengine, uhakika yakwamba Sheikh Muhammad bin Hādī al-Madkhalī al-Madanī, ambaye ni mwalimu katika Chuo Kikuu Cha Ki-Islamu Cha Madinah akitoa tahadhari dhidi yake [*yaani;* Sheikh Sālih as-Sindī] na "Daurah" zake zitakazofanyika Dubai? Baadhi ya vijana wameisambaza tahadhari hiyo isiyokuwa na dalili yoyote ya wazi na ushahidi, na kwa kweli suala hili lilinipa dhiki kubwa na nikahuzunika na tabia ya Sheikh Ibn Hādī, namuomba Allâh amsamehe. Kama ambavyo mimi sidhani kuwa imefichikana kwa yoyote asiyekuwa mimi yakwamba Dubai ni Mji mkubwa wa ki-Biashara ulio wazi kwa mtu yoyote binafsi, vikundi vya watu, mapote mengi, Dini tafauti, Madh-hebu nyingi, wenye ushawishi wa kila aina, mfumo wa Dini ya kisheriya, wasiokuwa na Dini, ma-biashara kila sampuli, usanii na hata michezo kutoka katika kila pembe ya ulimwengu. Kwa kiyasi cha kwamba mji huo umefungua kiwanja cha ndege cha kimataifa ambacho ni miongoni mwa viwanja vikubwa zaidi ulimwenguni na kinachopokea mamilioni ya watu – kwahivyo, *wallâhi,* sielewi ni vipi Sheikh Muhammad ibn Hādī anaweza kumuhadharisha Sheikh wa Aqîdah mfano wa Dr Sālih as-Sindī?!

Walillâhil-hamd, mimi kwa kawaida hufanya mawasiliano kwa njia ya barua kabla ya kumkosoa mtu kadiri ya uwezo wangu, basi nikajiuliza nafsi yangu; iwapo mimi nitawasiliana na Sheikh Ibn Hādī kwa njia ya barua, labda anaweza kuisoma na akanijibu, hususan kwa vile sasa yeye ni mgonjwa na kitambo kidogo hivi alifanyiwa upasuaji wa moyo, Allâh ampoze, pengine, na labda huwenda ikawa, barua yangu itamuathiri na atajiepusha na kutahadharisha dhidi ya Ahlus Sunnah. Kwa ajili hii, nikampelekea yeye barua hii ifuatayo:

Kutoka kwa Sālim bin Sa'd at-Twawîl, Kwa ndugu yangu, Dr. Sheikh Muhamamd bin Hādee:
As-salāmu alaykum wa rahmatullāhi wa barakātuhu, hapana madhara, insha-Allâh (itakuwa) Twahara. Muheshimiwa Sheikh, kama ilivyo sasa hivi yakwamba wewe ni mgonjwa, inakuwa ni fursa kwako kuzingatia baadhi ya matamshi yako kuwahusu Ahlus Sunnah na umche Allâh ndani ya nafsi yako. Wewe umewadhulumu wengi wao, akiwemo mwishoni mwao, kama ilivyopokewa kutoka kwako kwa kuwatahadharisha watu dhidi ya Sheikh Sālih as-Sindee. Kwani kwa hakika wewe umewazuiya watu wasifaidike kutoka kwake kwa sababu zisizojulikana.

Alinijibu kwa kusema: ***Wa 'alaykum salām wa rahmatullāhi wa barakātuhu,***

Ammâ ba'd

Iwapo umenielewa niliyoyasema, basi niwie radhi,
Au wajua uliyoyasema, basi mimi nakulaumu wewe:
Hata hivyo, wewe hukuyaelewa maneno yangu,
Na kisha nikajua yakwamba wewe ulikuwa ni mjinga, kwahivyo nimekupa udhuru.

Ulimi wangu, walillâhil-hamd, haufunguliwi isipokuwa kuzungumza kuwahusu watu wazushi, wenye kufuata hawaa', upotofu na wenye kuwatetea au kuwapa udhuru, hata kama anadai, au anadaiwa, yakwamba yeye ni miongoni mwa Ahlus

Sunnah. Kwahiyo, Sunni wa kiweli hakasirishwi kwa [haki] juu ya Ahlul Bid'ah na hawaombei udhuru, licha ya kuwatetea au kuwatia hima kufaidika kutoka kwao. Nakuombea kwa Allâh akupe ufahamu wa Dini Yake na akuonyeshe haki na akufugulie kifua chako, as-salāmu 'alayk.

Nikamjibu, kwa kusema:
Nakushukuru kwa unyenyekevu wako katika kunijibu, Allâh akuzidishie kheri. Na nakushukuru kwa kunipa kwako udhuru juu ya ujinga wangu. Juu ya yote hayo, haikufichika kutoka kwako yakwamba ni Allâh peke yake ndiye ajuae yaliyofichikana, ikiwa Sheikh Sālih as-Sindee anawatetea watu wa uzushi, wewe hukutubainishia sisi ushahidi wako ulio wazi ili upate kutuondolea ujinga wetu. Mimi nahofia yakwamba ulikuwa na pupa kama ulivyonishutumu pindi uliposema "Ikiwa Sālim at-Twawîl ni Simba miongoni mwa Simba wa Sunnah basi hapana usalama juu ya Suunah." - Ni kwanini? Kwani mimi ni Rāfidhi au Khārijî?

Mwisho wa mawasiliano yetu:

Mimi nasema: Nilimsubiri kwa masiku kadhaa aniletee ushahidi wa wazi na dalili na anibainishie kisawa sawa ni kina nani hao watu wazushi, wenye kufuata hawaa na wapotofu? Na ni kina nani hao wenye kuwatetea hao? Na ni kina nani wenye kuwatafutia udhuru hao? Na ni kina nani ambao si miongoni mwa Ahlus Sunnah ambao waliodai, au ikadaiwa yakwamba wao ni miongoni mwa Ahlus Sunnah? Na ni kina nani wenye kukasirika [katika kuwatetea] Ahlul bid'ah na kuwatafutia udhuru? Na ni kina nani wenye kuwatetea ahlul bid'ah na kuhimiza yakwamba watu wakanufaike kutoka kwao? Sisi hatujui mambo yaliyofichikana, twasubiri jawabu lako Ewe Sheikh Muhammad, na ni kutokamana na haki zetu yakwamba tunakuuliza utoe dalili za wazi.

« قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ »

"Sema, 'Leteni dalili zenu, kama nyinyi ni wasema kweli." [al-Baqarah 2:111]

Wakati Allāh (سبحانه وتعالى) alipowaumba Majini na wanaadamu na akawaamrisha wamuabudu Yeye peke yake pasi na mshirika, alitaja mamiya ya ushahidi wa wazi na dalili za Upweke wake. Allâh alipompeleka Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم), alimsaidia kwa mamiya ya Âyât zenye kuashiriya utume Wake na ujumbe Wake, sasa utawatakaje watu wategemee maneno yako pasi na ushahidi na dalili?! Ewe Sheikh Muhammad, watu wa Emirates sio kama watu wa Uropa, ambao unaowapeleka kama utakavyo na wanaokubali kila neno unalolisema bila ya dalili na wanaokubali jarh yako moja kwa moja na kwa unyenyekevu wa hali ya juu. Watu wa Emirates sio kama watoto wenye kuyakubali mipaka ya miondoko yako pindi tu pale inaposambazwa.

Ulikuwa wapi wewe, wakati al-Jifrī alipokuwa akitembea kuizunguka Emirates nzima?! Wewe ulitoa onyo dhidi ya al-Kubaysī wa madh-hab ya Mu'tazilah?! Aliyekuwa akiwalaani Maswahaba na alikuwa kwenye kipindi cha Kituo cha runinga cha Gulf Arabic channel, katika mji wa Dubai na kwengineko?! Mbona hatusikii hata neno moja

kutoka kwako kumuhusu [Twâriq] as-Suwaidān, aliyekuwa akifuliza safari zake kwenye nchi ya Emirates na akihudhuria vikao vya Daurah na akieneza alichokuwa apendacho katika mifumo ya Ikhwānī na fikra zao. Kwanini wewe unajisimamisha mbele ya Ahlus Sunnah, na hususan ma-Salafi? Unajua yakwamba wewe unawataifisha Ahlus Sunnah kwa kujiingiza baina yao?!

Wewe, haswa, ni kwanini unajiingiza kwenye mas'ala ya Emirates haliyakuwa wale wenye umri mkubwa, 'ilmu, makadirio na nafasi nzuri kukushinda wewe, hawajiingizi; kama vile Sheikh al-'Allāmah al-Muftī 'Abdul'Azeez Āli Sheikh, Sheikh al-'Allāmah Sālih bin Fawzān al-Fawzān, Sheikh al-'Allamah 'Abdulmuhsin al-'Abbād, Sheikh al-'Allāmah Sālih al-Luhaydān, Sheikh al-'Allāmah Rabī' al-Madkhalī na wengineo ambao wasiopungua umri wa miaka thamanini au chini yake. Ambapo wewe, kwa masikitiko, unaandaa kikosi cha watoto au baadhi ya vijana wadogo kusababisha mtafaruku na shaka? Unajua wewe yakwamba vitendo vyako vimewahamasisha ndugu wa ki-Salafi mbele ya waliokuwa na majukumu ya mas'uliya yao [*yaani; viongozi wao*] na mbele ya watu wenye kusubiri kupata faida kutoka kwa Mashekhe wa ki-Salafi na wanafunzi wa ki-Ilimu kama njia mbadala kwa watu wa uzushi na wenye kufuata hawaa?

Watu wa Emirates wana kiu na 'ilmu, Sunnah na 'Aqîdah swahîh baada ya Ikhwân kuvuna uharibifu kwenye nchi yao, na baada ya al-Jifrî kutaga aliyoyafanya, na baada ya al-Kubaysī kupanda (kumeza) aliyoyafanya, na baada ya as-Suwaydān kuvumbua aliyoyafanya. Tabiya yako, na tabiya ya vijana wako imesababisha unyanyasaji juu ya ma-Salafi. Bali, vitendo vyako vimewapa tena nguvu ma-Ikhwân na ma-Sufi iwapo unafahamu hayo au hufahamu! Naapa kwa Yule ambaye roho yangu iko Mkononi mwake, mimi sijawahi kuwasikiya ma-Imâm wa ki-Salafi wa zama zetu hizi wakifanya mambo uyafanyayo wewe. Kwani wao, Sheikh al-'Allāmah al-Muftī 'Abdul'Azeez bin Bāz, Sheikh al-Muhadith Muhammad Nāsiruddeen al-Albānī, Sheikh wetu, Faqeeh, Muhammad bin Sālih al-'Uthaymeen, Allâh Awarehemu, walikuwa wakiyakataa makosa na badala yake wakiwanaswihi wenye kukosea na wakiwaongoza. Hatahivyo, wao hawakuwa wakiwafuatilia Ahlus Sunnah kutoka mahali kumoja hadi kwengine na kutoka nchi moja hadi nyengine; na 'ilmu zao na wasifu zao zingali zimehifadhiwa *walillâhil-hamd* regelea kwenye kumbukumbu hizo ufaidike.

Ewe Sheikh Muhammad bin Hādee, wewe wajua yakwamba kuna waliokutangulia wewe katika kwenda nchi ya Emirates wakifundisha vitabu vya 'Aqîdah ya Salaf na wakiwatanabahisha kuhusu ma-'Ulamaa' wa Ahlus Sunnah na vitabu vyao na nukuu zao, na kwa matokeo yake vijana wengi wakaipenda Manhaj Ya Salaf? Kwanini unakuja sasa kuwazuiya haliyakuwa Allâh Ameleta manufaa makubwa kwa kupitia kwao? Kwanini huzikubali fadhla za wale waliokuwa kabla yako kama ambavyo Ibn Mālik alivyozikubali fadhla za Ibn Mu'tī? Kwanini unaharibu sifa zao bila ya dalili yoyote?!

Mche Allâh, Ewe Sheikh Muhammad, iwapo kuna tafauti zozote za ki-binafsi au uchunguzi wa mas'ala ya kisheriya baina yako na baadhi ya Mashekhe, basi tuheshimu sisi kwa kufunga mdomo wako na ukayasuluhishe mas'ala yaliyo kwenye nchi yako na uwachane na Emirates kabisa. Njia yako inawafanya wageni wayakimbie makaribisho

yoyote katika siku za mbeleni kutoka Emirates au mahali kwengine kokote na badala ya al-Jifrī mmoja watazuka maelfu ya kina al-Jifrī, na badala ya al-Kubaysī mmoja watazuka maelfu ya kina al-Kubaysī, na badala ya Suwaydān mmoja watazuka maelfu ya kina Suwaydān. Na sio mbali tena yakwamba vita vyako na Ahlus Sunnah vitaiongezea nguvu Ikhwânul Muslimîn, na hili ni jambo ambalo lililochunguzwa na kufuatiliwa kukuhusu wewe na wanafunzi wako.

Nchi ya Emirates kwa sasa ina wanafunzi wa ki-ilimu waliosoma na kuhitimu kutoka kwenye Vyuo Vikuu vya Shari'ah na miongoni mwao kuna wale wenye shahada za Daktari za matokeo ya daraja ya juu, *walillâhil-hamd,* na wana mafungamano na Mashekhe na ma-'Ulamaa' wenye kuwapa naswaha kuhusu rai zinazotokamana na wao wenyewe. Wale wenye hatamu za majukumu katika nchi ya Emirates vilevile wamekuwa na tahadhari mno na kuweza kupambanua baina ya mwenye kuleta uharibifu na mwenye kurekebisha, na wao ndiwo wa kwanza waliotoa tahadhari dhidi ya Ikhwânul Muslimîn.

Mimi nasisitiza na kusema: Sio mbali tena yakwamba katika kuwafuatilia kwako Ahlus Sunnah, wewe na watoto wako au vijana, kutawapa nguvu ma-Ikhwân, ambao hakuna aliyewafichua wao isipokuwa ni Ahlus Sunnah peke yao. Hii ni nukta muhimu, kwahivyo kuwa muangavu.

Namuomba Allâh atupe sote ufahamu wa Dini Yake na atuonyeshe haki na atufungue nyoyo zetu [kwenye hiyo haki] na atuokoe kutokamana na uovu wa nafsi zetu wenyewe na matukio ya uovu wa vitendo vyetu na atupe ikhlâs katika maneno na vitendo vyetu.

Kila sifa njema inamstahiki Allâh mwanzoni, mwishoni, kwa dhahiri na kwa siri, na twamuomba swala, amani na baraka zimshukie Mtume Muhammad, jamii yake na maswahaba zake wote.

Sheikh Sālim at-Twawîl, *"Risālah Lam Yahmiluhā al-Bareed ilā Sheikh Muhammad bin Hādee, hafidhahullāh* [Barua ambayo isoweza kutumwa kwa Posta kwa Sheikh Muhammad bin Hādee, Allāh Amuhifadhi]. Tarehe 30 Dhu'l-Hijjah 1435 AH/24 2014 CE, angalia kwenye kiungo hiki:

http://www.saltaweel.com/articles/366

Tafsiri kwa mukhtasari: 'AbdulHaq al-Ashanti

Tafsiri kwa Kiswahili: Abu Farida Muhammad Basawad

The Qur'an And Sunnah Society od East Africa. [QSSEA]

Mombasa, Kenya